

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA ISHIRINI NA TISA

14 MEI, 2026



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA ISHIRINI NA TISA – TAREHE 14 MEI, 2026

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa

Majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

337. MHESHIMIWA SALEHE MBWANA MHANDO (KILINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga madaraja yaliyoharibika katika maeneo mbalimbali ya Jimbo la Kilindi ili kurahisisha usafiri.

338. MHESHIMIWA MARY DANIEL SURATI (SERENGETI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha Halmashauri ya Serengeti inapata *Service Levy* kutokana na shughuli za Utalii Wilayani humo.

339. MHESHIMIWA GEORGE NATANY MALIMA (MPWAPWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Vituo vya Afya katika Kata za kimkakati za Chunya, Berege, Godegode na Mlembule - Mpwapwa.

340. MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESHER KABATI (KILOLO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya Kata ya Kimara na Idete - Kilolo.

OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

341. MHESHIMIWA THOMAS MGONTO KITIMA (IKUNGI MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, lini Serikali itakamilisha Sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Uwekezaji wa Umma nchini.

WIZARA YA FEDHA:

342. MHESHIMIWA KAFITI WILLIAM KAFITI (ILEMELA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, lini Serikali itaandaa Kanuni za Bima za lazima ili kutekeleza Sheria ya Fedha ya Mwaka 2022 na kuongeza Mapato ya Serikali.

WIZARA YA KILIMO:

343. MHESHIMIWA KIZA HUSSEIN MAYEYE (KIGOMA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali imechukua hatua gani za kuchochea Viwanda vya kuongeza thamani ya zao la Chikichi ili kupunguza uagizaji wa mafuta ya kula nje ya nchi.

344. MHESHIMIWA KHALID MUSSA NSEKELA (KYERWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha pembejeo, huduma za Ugani, bei na masoko ya uhakika ya Kimataifa kwa zao la Kahawa katika Jimbo la Kyerwa.

WIZARA YA UJENZI:

345. MHESHIMIWA DANIEL AWACK TLEMAI (KARATU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Njiapanda - Mang'ola - Matala ili Wakulima waweze kusafirisha Mazao yao kipindi cha masika.

346. MHESHIMIWA JOHN STEPHANO LUHENDE (BUKENE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza utekelezaji wa ujenzi wa Barabara kwa kiwango cha lami kutoka Nzega - Itobo - Igusule hadi Kagongwa.

V. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**DODOMA
14 MEI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE**